TANGAZO LA SERIKALI Na. 720 la tarehe. 16/8/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1)(a))*

SHERIA NDOGO YA KILIMO CHA MCHIKICHI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Kilimo cha Mchikichi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Afisa Ugani" maana yake ni mtaalam wa Kilimo, katika ngazi za wilaya, kata na kijiji;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu;

"kilimo" maana yake ni shughuli yoyote ya uzalishaji mali inayofanywa na binadamu na inajumuisha kilimo cha mazao, ufugaji wa wanyama hai, nyuki na samaki;

"mkulima" maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na uzalishaji au kilimo cha mazao ya chakula, biashara na matunda; na

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Kasulu au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

Wajibu wa Halmashauri

4. Halmashauri itakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kuweka mabango kwenye kila kijiji yanayoeleza kanuni bora za kilimo zinazopaswa kuzingatiwa na mkulima kwa mazao yanayolimwa kwenye eneo hilo;

(b) kuanzisha kitalu cha miche bora ya michikichi isiyopungua milioni moja au zaidi;

(c) kuhakikisha upatikanaji wa maafisa ugani katika kila kijiji;

(d) kuhamasisha wananchi kulima zao la mchikichi kwa ajili ya kujiongezea kipato;

(e) kuhakikisha viongozi wa serikali, na wadau wengine wanashiriki ipasavyo katika kuendeleza kilimo cha michikichi;

(f) wakulima wa michikichi wanasajiliwa pamoja na idadi cha ekari walizolima;

(g) kushindanisha wakulima bora na maafisa ugani bora katika vijiji, kata na hatimaye Halmashauri; na

(h) kusimamia uapatikanaji wa mbolea na pembejeo nyingine za kilimo.

Wajibu wa Serikali ya Kijiji

5. Serikali ya Kijiji itakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kuhakikisha inatenga ardhi kwaajili ya kilimo cha michikichi.;

(b) kwa kushirikiana na uongozi wa kitongoji inawezesha wakazi kupata ardhi ya kutosha kwaajili ya kilimo;

(c) kwa kushirikiana na uongozi wa kitongoji itahakikisha kuwa inahamasisha wananchi kulima zao la mchikichi kwa ajili ya kujiongezea kipato;

(d) kuhakikisha kuwa kila mkazi katika eneo la kijiji anayemiliki ardhi ya kilimo na mwenye uwezo wa kufanya kazi analima zao la mchikichi angalau ekari moja.

Wajibu wa Afisa Mwidhiniwa au Afisa Ugani

6. Afisa mwidhiniwa au Afisa Ugani atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba kila mkulima wa

zao la mchikichi-
(a) anaandaa mashamba kwa wakati;
(b) anapanda miche bora kwa mstari;
(c) anazingatia nafasi inayotakiwa kitaalam;
(d) anaweka mbolea kwa viwango na kwa wakati; na
(e) anapalilia kwa wakati palizi mbili au zaidi.

Wajibu wa atendaji wa Vijiji na Kata

7. Kila Afisa Mtendaji wa Kata na Kijiji atawajibika kutunza kumbukumbu za wakulima na mashamba ya michikichi yaliyomo katika kata au kijiji chake na atasimamia moja kwa moja utekelezaji wa Sheria ndogo hii.

Wajibu wa mkulima

8. Mkulima wa zao la mchikichi atakuwa na wajibu ufuatao:
(a) kupalilia shamba lake kwa wakati stahili isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo;
(b) kuweka mbolea;
(c) kutoa taarifa kwa Halmashauri kwa njia itakayokuwa inafaa kuhusu kuwepo kwa ugonjwa wowote wa zao la mchikichi au kuwepo kwa wadudu waharibifu;
(d) kutumia pembejeo kwa kuzingatia maelekezo ya kitaalamu kila mwaka isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo na Afisa Ugani; na
(e) kuchukua hatua za kuangamiza wadudu waharibifu au kutibu magonjwa kama atakavyokuwa ameelekezwa na Afisa Ugani.

Ukaguzi

9.-(1) Afisa Mwidhiniwa akishirikiana na Afisa Ugani anaweza-
(a) wakati wowote kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi mpaka saa kumi na mbili kamili jioni kuingia katika shamba la mchikichi kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;
(b) kuingia katika kaya yoyote kuanzia saa moja kamili asubuhi mpaka saa kumi kamili jioni ili kukagua ghala la chakula kuona kama taratibu

za kuhifadhi chakula zinazingatiwa;
(c) kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote atakayevunja Sheria Ndogo hii; na
(d) kupanga ratiba ya kutembelea mashamba ya wakazi ili kujionea kama wanatekeleza wajibu wa kulima na kutunza mashamba kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Makosa

10. Mtu atakuwa anatenda kosa a chini ya Sheria Ndogo ikiwa-
(a) atazembea au kushindwa kutoa taarifa ya ugonjwa wa mazao
(b) ataingiza mifugo kwenye shamba la michikichi au kitalu cha miche;
(c) ataharibu kwa makusudi kitalu cha miche ya michikichi;
(d) atamzuia Afisa Ugani au Afisa Mwidhiniwa kufanya majukumu yake aliyopewa chini ya Shera Ndogo hii;
(e) hatovuna mazao yaliyoko shambani ambayo yamefikia wakati wa kuvunwa; na
(f) atafanya jambo lolote linaloathiri zao la michikichi.

Adhabu

11. Mtu atakayepatikana na hatia kwa kutenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote.

Kufifilisha kosa

12. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi elfu hamsini endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hii.

---

JEDWALI

---

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 12)*

---

FOMU YA KUKIRI KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ………. Mwaka ……….…… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Kilimo Cha Mchikichi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, niko tayari kulipa kiasi cha faini ninayodaiwa.
NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….
Jina……………………………..     Saini………………………
MBELE YANGU:
Jina:…………………………………..…………………….....
Saini……………………….…………………………..………
Wadhifa:…………………………………………………………
Tarehe……………………………………………………………

Mhuri wa Halmashauri ya umewekwa katika Sheria Ndogo hizi kwa kuzingatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 11/11/2022 mbele ya:-

JOSEPH KASHUSHURA RWIZA,
*Mkurugenzi mtendaji,*
*Halmashauri ya wilaya*
*Kasulu*

ELIYA CHARLES KAGOMA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya wilaya*
*Kasulu*

NAKUBALI,

**L.S**

Dodoma,
31 Januari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (Mb.),
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*,